**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI, KUHUSU MAJUMUISHO YA HOJA MBALI MBALI ZILIZOTOKANA NA MJADALA WA BAJETI ZA KISEKTA KWA BAJETI YA MWAKA 2017/2018

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia neema ya uhai na kutuwezesha kukutana tena leo hii, tukiwa wazima wa afya ili kutekeleza wajibu wetu wa kuwatumikia wananchi. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu kwa niaba ya Kamati yangu ya Bajeti, ili niweze kutimiza sehemu ya majukumu ya Kamati yangu yanayotokana na maelekezo ya Kanuni ya 100(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, kwa kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu taarifa ya majumuisho ya Kamati ya Bajeti kuhusu mjadala wa Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inamshukuru sana Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, kwa kukubali mwaliko wa Kamati kuhudhuria katika kikao cha majumjisho. Aidha, Kamati yangu inathamini hekma, busara na mchango wake alioutowa wakati wa kikao hicho zilizosaidia kutatua changamoto iliyozojitokeza wakati wa kikao hicho, ambayo kimsingi sisi kama Kamati inayofanya kazi kwa niaba yako na Baraza lako hazikutufurahisha.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii, kuwapa pole wananchi wote wa Zanzibar walioathirika kutokana na mvua za masika ambazo ziliathiri sana miundombinu ya barabara, watu pamoja na mali zao. Aidha, napenda pia kuwapa pole wote waliopata athari kutokana na upepo mkali uliovuma katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu na kusababisha hasara kubwa kwa wananchi, kwa kuharibikiwa na nyumba zao, nawaomba wananchi wote walioathirika kwa namna tofauti wawe na subra, na tunamuomba M/Mungu awape unafuu kutokana na mitihani hiyo (Amin).

**Mheshimiwa Spika,** tokea tarehe 10, Mei Baraza hili limekuwa katika kipindi muhimu cha mjadala wa bajeti, ambapo bajeti za Wizara zote kumi na tatu (13) zimewasilishwa na kujadiliwa na Wajumbe. Mheshimiwa Spika, napenda kuikumbusha Serikali michango na hoja mbali mbali ambazo Wajumbe wamezitowa hazikuwa na dhamira ya kuikwamisha Serikali wala kuikandamiza, badala yake zilikuwa katika hali ya kutekeleza wajibu wa kikatiba wa chombo hichi wa kuisimamia na kuishauri Serikali, kwa dhamira chanya ya kujenga ili kuifanya bajeti yetu iwe bora zaidi, na iwanufaishe wananchi, ambao ndio tunao watumikia. Hivyo, kwa dhati kabisa, napenda kuchukuwa fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu, kwa namna walivyotekeleza wajibu wao huo, kwa kuzichambua bajeti za Wizara zote pamoja na kuishauri Serikali juu ya namna bora ya utekelezaji wake, kwa hakika michango yao na ushauri wao umekuwa na umuhimu mkubwa katika kuhakikisha bajeti ya Serikali inaleta tija kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Shukurani maalum ziwaendee Wajumbe wa Kamati yangu ya Bajeti, kwa ushirikiano wao waliouonesha na kazi kubwa waliyoifanya ya kuchukua hoja mbali mbali za kibajeti zilizotokana na mijadala ya bajeti, ambazo Kamati yangu imezifanyia kazi. Kwa hakika kazi hiyo haikuwa rahisi hata kidogo hasa kwa kuzingatia kwamba michango iliyotolewa ni mingi na yote ilikuwa na umuhimu mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba nizitilie mkazo shukurani zangu kwa kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo;-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mohammed Said Dimwa | Mwnyekiti |
| 2. | Mhe. Bahati Khamis Kombo | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Shehe Hamad Mattar | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Abdalla Ali Kombo | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Zulfa Mmaka Omar | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Asha Abdalla Mussa | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Simai Mohammed Said | Mjumbe |

Aidha, Kamati yangu ilisaidiwa kwa karibu sana na Makatibu wawili

1. Ndg. Abdalla Ali Shauri na
2. Ndg. Kassim Tafana Kassim

**Mheshimiwa Spika,** itakumbukwa kwamba marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2016, pamoja na mambo mengine yalianzisha Kamati ya Bajeti. Aidha, Kanuni ya 100(2) ya Kanuni hizo, inaelekeza Serikali kwa kushirikiana Kamati ya Bajeti kufanya majumuisho kuhusiana na hoja mbali mbali zitakazojitokeza wakati wa mjadala wa Makadirio ya bajeti za Wizara zote.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati yangu imetekeleza jukumu hilo, kwa umakini mkubwa ambapo kwa muda wote wa majadiliano ya bajeti imekuwa ikifanya kazi ya kukusanya hoja mbali mbali zilizotokana na michango ya Wajumbe pamoja na maoni ya Kamati za kisekta, yaliyowasilishwa Barazani kupitia taarifa zao. Kwa msingi huo Kamati yangu ilipata fursa ya kukaa pamoja na Serikali kwa lengo la kushauriana kuhusu hoja zilizojitokeza wakati wa mijadala ili kuangalia maeneo ambayo yanaweza kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza au kupunguza sehemeu ya fedha zilizokadiriwa au kushauri mikakati ya utekelezaji wake. Hivyo, taarifa hii ni mrejesho kwa Baraza lako tukufu juu ya matokeo ya mashauriano hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kulikamilisha zoezi la majumuisho Kamati yangu ilikaa pamoja na Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohammed, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndg. Khamis Mussa Omar, pamoja na baadhi ya Watendaji wakuu wa Wizara hiyo. Aidha, Kwakuwa hoja zilizojadiliwa na Kamati yangu zilihusu Wizara tofauti, kwa lengo la kupata ufafanuzi zaidi katika kikao cha mashauriano, Kamati yangu iliwaita Mawaziri wa Wizara zilizohusika na hoja ambao nao pia waliambatana na watendaji wakuu wa Wizara hizo ili kuweza kusaidia kutoa ufafanuzi wa hoja zilizoibuka.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuthamini umuhimu na michanago ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Kisekta, Kamati yangu pia iliona ni busara kuwaalika Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Kisekta za Baraza. Hivyo kwa dhati kabisa Kamati yangu inawashukuru Wenyeviti, mawaziri pamoja na watendaji wakuu wa Wizara walioambatana na mawaziri kufika mbele ya Kamati kutoa ufafanuzi wa hoja ambao uliisaidia Kamati kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** naomba ifahamike kwamba, Kamati yangu imepata changamoto nyingi wakati wa kutekeleza jukumu hilo, pamoja na ukweli kwamba Kamati imepatiwa mafunzo ya kuijengea uwezo, hata hivyo mafunzo hayo hayakutosheleza kutokana na ukweli kwamba Kamati haikupata fursa kubwa ya kuona kivitendo, namna Kamati ya bajeti inavyofanya kazi, badala yake imepata mafunzo ya maelezo tu yaani"*theory*". Aidha, kutokuwepo kwa Sheria ya Bajeti ambayo kimsingi ingeweza kusaidia kuipa nguvu Kamati pamoja na kubainisha majukumu na mipaka ya vyombo mbali mbali katika mchakato wa bajeti, pia ni sehemu ya changamoto hizo. Kwa upande mwengine Kamati yangu ilikabiliwa na changamoto ya muingiliano wa ratiba ya kazi ambapo takribani kwa muda wa wiki nzima Kamati ililazimika kukosa kufuatilia mijadala ya bajeti za Wizaraza moja kwa moja kutokana na kupangiwa ratiba ya kupitia miswada mitatu yanayohusiana na masuala ya kodi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima kubwa naomba niwaarifu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Kisekta kwamba wanajukumu muhimu la kuipatia Kamati ya Bajeti changamoto za kibajeti za Sekta wanazozisimamia ambazo wanahisi zinahitaji nguvu na ufuatiliaji wa Kamati ya Bajeti. Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inalazimika kusema hivyo kutokana na ukweli kuwa Kamati za Kisekta ndio wanaojuwa zaidi uhalisia wa changamoto zilizomo katika Sekta wanazozisimamia, lakini pia wana nafasi kubwa ya kujuwa uzito wa changamoto hizo na kama zinahitaji kufikwishwa mbele ya Kamati ya Bajeti.

## YATOKANAYO NA MIJADALA YA HOJA

**Mheshimiwa Spika,** maeneo yaliyochangiwa ni mengi na kiujumla michango yote iliyotolewa ilikuwa muhimu na mizuri**, Mheshimiwa Spika,** Naomba ifahamike kwamba wakati wa kuchukua hoja zinazotokana na mjadala wa bajeti za kisekta Kamati yangu imejielekeza zaidi katika masuala ya bajeti na ambayo moja kwa moja yanahusu vifungu vya kibajeti. Aidha, Kamati pia ilizingatia baadhi ya hoja ambazo zilichangiwa na Wajumbe wengi kwa hisia kwa lengo la kupata maelezo zaidi kutoka kwa Serikali na kuweza kuishauri kuhusu utekelezaji wa maeneo hayo, kwakuwa baadhi ya maeneo hayo yanakosa ufanisi wa kiutendaji kutokana na changamoto za bajeti.

## Maeneo yaliyochangiwa na Wajumbe Wengi

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya maeneo yaliyochangiwa na Wajumbe wengi na kwa hisia zaidi ni pamoja na haya yafutayo**.**

1. Udhalilishaji wa kijinsia na umuhimu wa kuiengeza bajeti ya fungu hilo
2. Kutokuwepo Ufanisi katika utekelezaji wa Miradi mikubwa ya Kitaifa (Terminal II, na "E.Government", ).
3. Utekelezaji wa Ahadi za Viongozi Wakuu
4. Utaratibu mpya wa usimazi wa Uchimbaji Mchanga na bei elekezi za Serikali
5. Kuchelewa kukamilika miradi ya barabara
6. Umuhmu wa kutumia mifumo ya kisasa katika kukusanya mapato
7. Kutoridhishwa na Huduma za Hospitali ya Mnazi Mmoja
8. Nidhamu katika Matumizi ya Fedha za Serikali
9. Umuhimu wa kukuza ufanisi katika kukusanya mapato
10. Kukamilishwa mabanda ya skuli ambayo wananchi wameyajenga kwa nguvu zao.
11. Mikakati ya kukabiliana na maafa pamoja

## MAMBO YA MSINGI YALIYOBAINIKA

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa Mjadala wa bajeti za Kisekta Kamati yangu imebaini kwamba bado kuna changamoto nyingi za kibajeti katika taasisi nyingi za Serikali kutokana na mahitaji makubwa waliyonayo, ambapo taasisi nyingi zinashindwa kufikia malengo waliyojiwekea kutokana na ufinyu wa bajeti, mfano mzuri ni madeni ya vikosi vya Idara Maalum ambayo yanadaiwa na "*Supplier*" wao . Ili kukabiliana na changamoto hii Kamati yangu inaishauri Serikali kuongeza vyanzo vya mapto ili kuongeza uwezo wa Serikali katika kukusanya mapato. **Mheshimiwa Spika,** Ushauri zaidi kuhusu vyazo vya mapato ambavyo Serikali wanaweza kuvitumia ili kutanua wigo wa mapato utatolewa na Kamati yangu wakati wa kuwasilisha Houtuba ya maoni ya Kamati kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali.

## NIDHAMU KATIKA MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA:

**Mheshimiwa Spika**, Nidhamu ya matumizi ni msingi muhimu katika kuyafikia malengo ya mipango tunayojiwekea, iwapo suala la nidhamu ya matumizi halitozingatiwa, jitihada zetu katika kukuza mapato hazitokuwa na tija yoyote kwani itakuwa ni sawa na kuchumia kwenye mkoba mbovu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inalisema hili kutoka na namna jambo hili linavyoathiri bajeti ya Serikali. Aidha, hamu ya Wajumbe wengi kutaka kuichangia taarifa ya Ukaguzi maalum wa Ripoti ya Mdhibiti iliyowasilishwa ambao Mhe. Rais aligaiza kufanywa kuhusu mishahara hewa, umeonesha kwa kiasi gani Wajumbe wa Baraza lako hawaridhishwi na vitendo hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwakuwa Kanuni za Baraza zimeipa jukumu Kamati ya PAC kuifanyia kazi ripoti hiyo, tunaiomba Afisi yako iiwezeshe Kamati PAC kwa kuitengea muda wa kutosha ili iweze kuifanyia kazi ripoti hiyo na hatimnae iwasilishe ripoti yake hapa Barazani kwa muda muafaka, ili Wajumbe wapate kuichangia ripoti hiyo. Kamati yangu imelazimika kulitilia mkazo suala hili, kwakuwa ni ukweli kwamba, Kamati ya PAC inajukumu kubwa la kuifanyia kazi ripoti ya Mdhibiti ya kila mwaka kwa Wizara na Taasis

zote za Serikali pamoja na Mashirika, hivyo bila ya kutengewa muda wa kutosha Kamati hii haitoweza kuzifanyia kazi ripoti zote.

## UTEKELEZAJI WA AHADI ZA MHE. RAIS

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi walilalamikia suala la utekelezaji wa Ahadi za viongozi wakuu (Mhe. Rais pamoja na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais). Kamati yangu inaitaka Serikali kuzingatia na kuzipa umuhimu ahadi hizo wakati wa upangaji wa Bajeti kwakuwa nyingi kati ya ahadi hizo ni za muda mrefu, hali ambayo haileti taswira nzuri pia hali hiyo inaweza kupelekea wananchi kukosa imani na viongozi wetu.

## UFANISI MDOGO KATIKA KUKUSANYA MAPATO

**Mheshimiwa Spika,** Mapato ni sehemeu muhimu sana katika bajeti, hata hivyo pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuongeza mapato, imebainika kwamba bado kuna taasisi nyingi za Serikali hazifikii malengo katika kukusanya mapato, hali amabayo haileti taswira nzuri kwa taasisi hizo.

## USHAURI WA JUMLA

Kamati yangu inashukuru Baraza la Wawakilishi kwa kuanzisha utaratibu huu wa Serikali kufanya majumuisho ya mjadala wa bajeti ambao kimsingi unalipatia Baraza fursa pana ya kushauriana na Serikali kuhusu mwelekeo wa Bajeti na mgawanyo wa fedha. Kutokana na upya wa Kamati hii, Kamati yangu wakati wa kutekeleza jukumu hili gumu ilipata changamoto ya kutoeleweka na baadhi ya Wajumbe pamoja na baadhi ya watendaji ambao walikuwa na hofu kwamba Kamati hii ina lengo la kuizuia bajeti ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu imefanya kazi kubwa ya kujaribu kuwaelewesha Wajumbe kuhusu jukumu la Kamati hii. Hata hivyo, tunaiomba Afisi ya Baraza ichukue juhudi za makusudi kuandaa utaratibu maalum wa mafunzo kwa wajumbe wote wa Baraza kuhusu Kamati ya Bajeti, aidha mafunzo kama hayo yatolewe kila mara wakati inapoanzishwa Kamati mpya badala ya kuwasomesha Wajumbe wa Kamati husika tu

kuhusu majukumu ya Kamati yao, kwakuwa msingi wa utekelezaji wa Kamati hizo unategemea kwa kiasi kikubwa ushirikiano wa Wajumbe wote.

## UFAFANUZI WA HOJA ZINAZOTOKANA NA MAJADILIANO YA MAJUMUISHO BAINA YA SERIKALI NA KAMATI YA BAJETI

**Mheshimiwa Spika, Kwa msingi huo** Kamati yangu ilipata jumla ya hoja 34 kutoka katika mafungu tofauti zikiwemo hoja zinazohusu ukusanyaji wa mapato, hoja za kuongeza mafungu ya bajeti, hoja za kupunguza baadhi ya mafungu ambayo yana fedha nyingi, hoja za kutoridhishwa na utekelezaji wa baadhi ya programu pamoja na Hoja za jumla kuhusu utekelezaji wa bajeti ambazo zimechangiwa na wajumbe wengi.

**Mheshimiwa Spika**, ili kutowa urahisi wa ufafanuzi wa hoja zilizofanyiwa kazi na Kamati, Kamati yangu inaomba iwasilishe hoja hizo kwa njia ya Bango Kitita/Jadweli ambalo limegawika Sehemu Tatu; sehemu ya kwanza inahusu Hoja za Kisekta, Sehemu ya Pili inahusu, majibu ya Serikali na sehemu ya Tatu ni Ushauri wa Kamati ya bajeti.

| | **1.AFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS: FUNGU C01-C05** | | | |
|---|---|---|---|---|
| No | **HOJA** | **MAJIBU YA WIZARA** | **MAONI YA KAMATI** | **FEDHA ZILIZOON GEZWA** |
| 1. | Idara ya Watu Wenye Ulemavu kupitia programu ya usimamizi wa masuala ya watu wenye ulemavu bajeti yake ni ndogo sana kwa mujibu wa mahitaji ya Idara hiyo, na uhalisia wa shughuli zake za kila siku ambapo kwa mwaka wa fedha **2017/2018** | Kamati iliarifiwa Sababu ya kutofanyika kwa vikao hivyo ni kutopatikana kwa fedha kama ilivyotarajiwa. Pia vikao hivyo havikua kipaumbele kulinganisha na upatikanaji wa fedha.<br><br>Amabapo fedha zilizopatikana zilitumika | Maoni ya kamati ni kuwa fedha zilizopangwa ziingizwe kwa wakati ili idara iweze kutekeleza majukuu yake yote kwa wakati kama ilivyojipangia | Hakuna fedha zilizoongez wa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | imetengewa Tsh **498,832,240**. Aidha, Kwa mwaka wa fedha **2016/2017**, Baraza la watu wenye ulemavu halikupata kukaa hata kikao kimoja kati ya vikao vinne (4), vilivyokusudiwa, miongoni mwa sababu zilizopelekea kutofanyika kwa vikao hivyo ni pamoja na ufinyu na ucheleweshwaji wa bajeti, kati ya Tsh **462,121,000** Idara ilipata Tsh **103,461,6000** sawa na asilimia 22 tu ya makadirio. | kwa mafunzo, uhamasishaji na ununzi wa vifaa visaidizi, na ueneshaji wa ofisi.<br><br>Iwapo vikao hivvo ni kipaumbele ilibdi Mkurugenzi awasiliane na Katibu Mkuu ili kumtaarifu juu ya kipaumbele hicho na kianze kutekelezwa kwa mujibu wa upatikanaji wa fedha.<br><br>Hata hivo wizara imeahidi kuwa idara hii itapewa kipaumbele katika upatikanaji w fedha kwa bajeti ya mwaka 2017/2018.<br><br>Aidha idara imekiri kuwa, fedha hizo zilizotengwa, zitakidhi mahitaji ya idara. | | |
| 2. | Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya imepangiwa milioni **598,900,000**/- lakini Tume ya UKIMWI imepangiwa milioni **846,800,000**/-. Kutokana na umuhimu wa Mapambano dhidi ya Madawawa ya kulevya. Imependekezwa | Kamati iliarifiwa kwamba Tume ya Ukimwi ina maihitaji zaidi ya bajeti kutokana na kuwa ba wafanyakazi wengi kulinganisha na wafanya kazi wa Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya. | Kwa kuwa Mkrugeni wa Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya aliridhika na bajeti aliyopangiwa sambamba na ufafanuzi wa Wizara kuhusu mahitaji ya Tume hizo, Kamati imeridhia bajeti | Hakuna fedha iliyoengezwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | kwamba, bajeti iliyopangiwa Tume ya Ukimwi ipangiwe Idara inayohusiana na Udhibiti wa Madawa ya Kulevya, na bajeti ya madawa ya kulevya ije kwenye Tume ya Ukimwi. | Lakini pia utafiti uliofanyika mara ya mwisho unaonesha bado kuna ongezeko la maambukizi ya vurusi vya UKIMWI kwa jamii ya kizanzibar. Aidha, kwa sasa Tume ya UKIMWI inakosa wadhamini wa miradi ya maendeleo ambao kabla walikua na msaada mkubwa katika maswala ya kibajeti.<br><br>Lakini pia Tume ya Dawa zakulevya imeridhia kiwango cha fedha kilichopangiwa kwa mujibu wa mahitaji yao. | za tume hizo mbili zibakie kama zilivyo bila mabadiliko yoyote. | |
| 4. | Imependekezwa Bajeti ya Idara ya Sherehe na Maadhimisho pamoja na Kuwaenzi Viongozi Wakuu ambayo ni Tsh **1,081,975,600** ipunguzwe, ili fedha itumike katika kukabiliana na maafa na hasara iliyotokezea kutokana na mvua na upepo pamoja na kusaidia kutengeneza miundo mbinu ya barabara zilizoharibika | Kamati iliarifiwa kuwa kiuzowefu, bajeti inayopangiwa Idara hii, huwa haitoshelezi kwa uadhimishaji wa sherehe za kitaifa ikiwa ni pamoja na Sherehe za Mapinduzi, hivyo iwapo fedha zitapunguzwa, sherehe hizo hazitaweza kufanyika kama ilivyo kawaida.<br><br>Aidha fedha hizo haziwezi kutumika katika maafa, kwa | Kamati imeridhia baada ya kupatiwa ufafanuzi wa kina. | Hakuna fedha iliyoengezwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kuwa tayari kuna mfuko maalum wa maafa. Aidha hakuwezi kuwa na kiwango cha fedha maalum kwa ajili ya maafa, kwa kuwa hatuwezi kujua kitu gani kitatokea. | | |
| | | | | |
| | **AFISI YA RAIS IKULU:FUNGU A01- A02** | | | |
| 1. | Idara ya GSO ina mazingira magumu ya kiutendaji kazi kutokana na ufinyu wa Bajeti inayopangiwa ambapo kwa mwaka wa fedha **2017/2018** imepangiwa **TZS 75,000,000**. Tatizo hili pia linatokana na muundo wa Idara unaotokana na Sheria inayosimamia Idara hiyo. Aidha, utekelezaji wa Malengo wa Idara hiyo ni mdogo sana. | Wizara imekiri ni kweli Idara ina matatizo yanayochangiwa pia na sheria inayosimia Idara hiyo, lakini pia yapo matatizo yaliyopatiwa ufumbuzi ikiwa ni pamoja na suala la usafiri wa gari kwa Idara hiyo. Aidha, Kamati imehakikishiwa na Wizara kuwa bajeti iliyotengwa mwaka huu wa fedha inatosheleza mahitaji ya Idara hiyo.<br><br>Wizara pia imeanza kuchukua juhudu za kufanya mazungumza na upande wa pili wa muungano, na wamefikia hatua nzuri | Kamati imemshauri Mwenyekiti wa Kamati ya kisekta awe karibu na Wizara na kuhakikisha changamoto hiyo inaanza kufanyiwa kazi katika robo ya mwanzo ya bajeti ya mwaka 2017/2018 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | katika kuhakikisha tatizo linamalizika. | | |
| 2. | Kuhusu ahadi za Mhe. Rais ambazo hazijatekelezwa licha ya kuwa ahadi hizo ni za muda mrefu. | Wizara imeahidi itaendelea kuhimiza sekta husika ambazo zinahusika katika utekelezaji wa ahadi hizo ili zitekelezwe kwa wakati | Kamati ya kisekta imeagizwa kufuatilia utekelezaji wa jambo hili. | |
| 3. | Kuhusu suala la mishahara hewa, suala hili msingi wake ni ripoti ya Ukaguzi maalum alioufanya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutokana na agizo la Mhe. Rais, Wajumbe walilizungumzia kwa hisia namna linavyoathiri bajeti ya Serikali na kuitaka Serikali kuwachukulia hatua waliobainika kuhusika na kadhia hiyo | Kamati imeelezwa kuwa Suala hili bado linafuatiliwa, aidha kuna Kamati maalum iliyoundwa na Mhe. Rais, kufuatilia suala hilo na baada ya kukamilika taratibu, wanaohusika watachukuliwa hatua. | Kamati imeendelea kusisitiza kuchukuliwa hatua waliohusika, kwa mujibu wa sheria. | |
| | | | | |
| | **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:FUNGU G01-G09** | | | |
| 1. | Wajumbe wameishauri Serikali, kuhusu umuhimu wa Taasisi za Serikali kutumia Majengo yao wenyewe badala ya kukodi pamoja na kuyafanyia matengenezo | Kamati imeelezewa kuwa, Kuhusu jengo la Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Wizara tayari wameshahamia katika jengo lao jipya. | Kamati imeshauri kuwa, Mwenyekiti wa Kamati ya PAC, afanye ukaguzi wa jengo hilo, ili kuhakkiisha matumizi mazuri ya fedha za | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | (ukarabati) ili kulinda hadhi za taasisi za Serikali, lakini pia kuepuka upotevu wa fedha nyingi za Serikali kwa kukodi majengo: Mfano wa taasisi hizo ni Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Pemba ambao wanatumia jengo la kukodi. | | umma. | |
| 2. | Baadhi ya Wajumbe walijenga hofu ya kutoridhika juu ya ufanisi wa Mradi wa E-governemet, ambao mwaka huu unatarajiwa kutekelezwa kwa awamu ya pili na ambao kiujumla unagharimu Serikali fedha nyingi kwa mfano kwa mwaka wa fedha **2017/2018** jumla ya Tsh **10,000,000,000** za mkopo kutoka kwa wafadhili "Exim bank" na milioni **50,000,000** kutoka SMZ zimekadiriwa kwa ajili ya Mradi huo. | Wizara imeeleza baada ya ukamilika kwa awamu ya kwanza ya kuweka miunndo mbinu, awamu ya pili ya mradi imekusudia kutekelezwa katika maeneo ya "e-tax" na "e-health", ambayo ni mapya.<br><br>Kwa mujibu wa "scope" ya mradi, fedha hizo sio nyingi kama zinavyoonekana. Aidha kwa kuwa fedha hizo ni za wahisani, ambazo Serikali tayari imeshaingia makubaliano kwa ajili ya mradi husika, hivyo si busara kuzipunguza fedha hizo. | Kamati iliagiza kupatiwa "scope" ya mradi husika, ili kujiridhisha, na tayari imepatiwa uchanganuzi wa mradi huo. | Hakuna fedha iiyopunguzwa. |
| | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | **AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ: FUNGU D01-D09** | | | |
| 1. | Baadhi ya Wajumbe walichangia kuhusu Kiwanda cha Ushoni cha Kikosi cha Valantia, ambapo walikitaka kiwezeshwe ili kiweze kuzalisha viatu kwa kiwango kikubwa na kizuri. Aidha Wajumbe walipendekeza kikosi hicho kiongezewe Bajeti kwa kuwa bajeti ya maendeleo kwa mwaka 2016/2017, kwa kipindi cha miezi tisa kati ya Tsh **827,200,000** walipata Tsh **27,430,000** sawa na asilimia **3.3** tu ya bajeti iliyopangwa kwa kazi za Maendeleo. Hivyo, Wajumbe wamesisitiza kwa mwaka wa fedha **2017/2018** bajeti iliyopangwa ya **Tsh 400,000,000** wapatiwe kama walivyopangiwa. | Wizara imeeleza kuwa, fedha hizo tayari zimeshapatikana. Aidha kuchelewa kwa fedha hizo kulitokana na kuwa muda wa matumizi wa fedha hizo ulikuwa haujafika. | Kamati imeridhia baada ya kuelezwa kuwa fedha hizo zimepatikana. | |
| 2. | Makusanyo ya Chuo cha | Wizara ilieleza kuwa | Kamati imesisistiza | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Mafunzo kwa mwaka **2016/2017** hayaridhishi hususani Viwanda vya mafunzo ambapo hadi machi **2017** jumla ya Makusanyo yalikuwa TSh **2,419,000** sawa na asilimia **22** ya makadirio ya **Tsh 11,000,000** | makausanyo hayo yalikuwa ni kwa kipindi cha miezi 9, ambapo katika kipindi kilichosalia, mapato hayo yameongezeka | umuhimu wa taasisi za Serikali kusimamaia vyema vyanzo vya mapato ili kufikia malengo wanayojiwekea. | |
| 3. | Ili kuongeza ufanisi katika suala zima la mapato, Wajumbe wamependekeza Ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri utumie Mashine pamoja na njia ya Benki. | Wizara imeeleza kuwa imejipanga kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki, katika ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kama ni moja wapo ya mikakati ya utekelezaji wa dhana ya Ugatuzi. | Kamati inashauri Kamati ya Kisekta kulifuatilia suala hili na kuhakikisha linatekelezwa ndani ya mwaka wa fedha wa 2017/2018. | |
| 4. | Kuhusu ununuzi wa gari 2 za "Fire Airport" zilinunuliwa takriban **$ 3,400,000** Wajumbe wengi wameonesha kutoridhishwa na gharama za ununuzi wa gari hizo, kwa kuwa gharama zilizotumika ni kubwa sana. Aidha, Wajumbe wa **Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum** hawakupatiwa | Wizara imeeleza kuwa, "Specification" za gari hizo zipo, na kama zingehitajika zingepatikana.<br><br>Aidha, Kamati imearifiwa kuwa, kila gari moja, ilinunuliwa kwa gharama ya Dola laki 993.75 | Kamati imeomba kupatiwa "specification" hizo kwa ajili ya kujiridhisha na tayari vielelezo hivyo vimeshawasilishwa. | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | nyaraka za ununuzi wa gari hizo ikiwemo "*Specification*" zake. | | | |
| 5. | Kwakuwa baadhi ya vikosi vya Idara maalum ikiwemo Chuo cha Mafunzo vinadaiwa madeni mengi na watoa huduma "*supplier*" madeni ambayo kimsingi hayalipiki kwa fedha za OC wanazoingiziwa. Wajumbe wameshauri Madeni hayo yafanyiwe uchanganuzi, ili yale yasiyolipika, Kamati ya bajeti ikae na Wizara ya fedha kwa lengo la kuangalia mafungu mengine ambayo yanaweza kutumika kulipia madeni hayo | Wizara imeeleza kuwa, Ulipaji wa madeni ni jukumu la taasisi husika, kwa kutumia fedha wanazoingiziwa.<br><br>Madeni ya Taasisi ya muda mrefu na ambayo hayalipiki yatalipwa kwa kufuata utaratibu wa Serikali ambao unafahamika. | Kamati imeridhika na majibu ya Serikali. | |
| | | | | |
| | **I. WIZARA YA HABARI UTALII UTAMADUNI NAMICHEZO: FUNGU JO1-J02** | | | |
| 1. | Wajumbe wameitaka Serikali kufanyika jitihada zaidi ili kuhakikisha Mapato yatokanayo na Sekta ya Utalii yanaongezeka. Aidha mfumo unaotumika sasa hivi wa kukusanya takwimu za | Wizara imeeleza takwimu za Watalii zinapatikana kutoka kitengo cha takwimu cha Idara ya Uhamiaji, ambapo takwimu hizo zipo za aina bili,(watalii wanaotoka moja kwa moja | Kamati imeshauri utumike utaratibu wa aina moja wa ukusanyaji wa takwimu kwa "airport" na bandarini, lakini pia ukusanyaji wa takwimu | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | watalii Bandarini na katika viwanja vya ndege, ambao hutegemea taarifa za takwimu kutoka Idara ya Uhamiaji ubadilishwe. | kutoka Tanzania bara na wanaotoka moja kwa moja kutoka nje ya nchi). Na kwa sasa takwimu zote hizo zinakusanywa. Aidha, Idara inajiandaa kuanza kutumia mfumo wa "Digitali".<br><br>Hivi karibuni Wizara imekaa na kampuni ya "Azam Marine" kwa lengo la kujadiliana juu ya namna ya kuboresha ukusanyaji wa takwimu. | hizo ujumuishe hata watalii wa ndani wanaokuja Zanzibar kutoka Tanzania Bara. Aidha, ukusanyaji wa takwmiu hizo usiandaliwe katika mazingira ambayo yatawasumbua watalii, na pia inashauriwa kuwa kuandaliwe fomu za kujaza wageni za kutambua wanakotoka, kabla ya kushukua katika chombo cha usafiri ndege au boti. | |
| 2. | Kutokana na umuhimu wa Sekta ya Utalii, Wajumbe pia wameshauri bajeti ya kuutangaza utalii iongezwe ili utalii wa Zanzibar uweze kutangazwa zaidi na kuongeza Idadi ya Watalii wanaokuja Zanzibar. Ambapo bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha **2017/2018** ni **Tsh 425,293,000** tu | Wizara imeeleza kuwa, tatizo si kuutangaza utalii pekee, lakini pia kuwafanya watalii kubaki Zanzibar na kushawishika kurudi tena. Aidha kuna jumla ya Tsh. Bilioni 1, zilizotengwa kwa ajili ya uboreshaji wa maeneo ya kihistoria.<br><br>Pia Kamati imearifiwa kuwa, fedha zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018, zinatosha | Kamati inashauri kuwa, Wizara isitosheke na dhana kuwa Zanzibar ni "Brand" inayojiuza yenyewe kweye soko la utalii, kwani hata nchi zilizopiga hatua kubwa kwenye sekta ya utalii, bado zinaendelea kutangaza nchi zao kwa gharama kubwa, ili kuenda sambamba na ushindani unaoendelea kuongezeka katika soko | Hakuna fedha iliyoongez wa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kulingana na malengo waliyojiwekea.<br><br>Aidha, wizara imejipanga kuishirikisha sekta binafsi katika kuitangaza Zanzibar kiutalii kupitia maonesho mbali mbali. | la utalii. | |
| 3. | Wajumbe wengi hawakuridhishwa na ukusanyaji wa mapato wa Wizara ya Habari katika Programu ndogo ya Uimarishaji wa Utalii na Maeneo ya kihistoria ambapo kwa mujibu wa ripoti ya Kamati, kwa mwaka wa fedha **2016/2017** jumla ya Tsh **170,110,202** zilikusanywa sawa na asilimia **43** tu ya lengo la makusanyo ya Tsh **392,268,000**. | Wizara imeeleza kuwa, kuharibika kwa jengo la **Bait la Jaib,** pamoja na uharibifu uliotokea katika jengo la **"People's Palace"** ni miongoni mwa sababu zilizopelekea kupungua idadi ya watalii na mapato. | Kamati imeshauri jitihada zaidi ziongezwe katika kusimamia na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria pamoja na kubuni vianzio vipya vya mapato vilivyomo katika taasisi zinazohusika na programu hiyo | |
| | | | | |
| | **WIZARA YA UWEZESHAJI, WAZEE, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO: FUNGU Q01** | | | |
| 1. | Wajumbe wengi waliochangia Wizara hii waligusia kifungu cha Mapambano dhidi ya Udhalilishaji wa Watoto | Wizara imeeleza kuwa Wizara imefanikiwa kukaa na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari, na kuifanyia kazi hoja hiyo na | Kamati imepongeza uamuzi huo, ambao umeonesha kujali na kuthamini maoni ya | Fedha zilizoongezwa ni **120,000,00** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | ambacho kilitengewa **Tsh 55,100,000** milioni tu. Wajumbe walitaka kifungu hichi kiongezewe fedha ili kiende sambamba na hali halisi ya tatizo la udhalilishaji katika nchi yetu ikiwa ni njia moja wapo ya kusaidia harakati za kupambana na vitendo hivyo. | kukubaliana na mabadiliko yafuatayo:<br><br>Kifungu SQ **010202** programu ndogo ya Mapambano dhidi ya udhalilishaji wa Wanawake na watoto chenye shilingi **55,100,000/** kiongezwe fedha hadi kufikia shilingi **175,100,000** ambazo ni sawa na ongezeko la shilingi **120,000,000** ambazo ni sawa na asilimia **69%** ya makadirio.<br><br>Aidha, mapendekezo yaliyofikiwa fedha hizo zitoke katika vifungu vifuatavyo:<br><br>a. Fungu **SQ010201** Programu ndogo ya Uratibu wa Masuala ya Kijinsia na Uendelezaji Wawanawake shilingi **80,000,000/**<br>b. Fungu **SQ010301** Programu Ndogo ya Uratibu wa Huduma za Uhifadhi ya Jamii | wajumbe wa Baraza. | 0 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | shilingi **40,000,000/-** | | |
| 2. | Wajumbe wengi walichangia kuhusu utaratibu wa pencheni za Wazee waliofikia miaka 70 kwamba hauko vizuri, ambapo baadhi yao hawajafikia mika 70 wanalipwa kwasababu walijiandikisha na baadhi yao wamefikia miaka 70 lakini hawalipwi kwasababu hawajajiandikisha. Aidha, utaratibu wa kuwafuta wazee waliofariki na kuwaingiza wazee wapya hauko wazi. Kutokana na hali hiyo, Wajumbe wamejenga hofu ya kwamba fedha zinazotengwa kwa ajili ya zoezi hilo hazitumiki vizuri. | Wizara imekiri kuwepo kwa tatizo hilo, na wameiarifu kamati kwamba wamepanga mikakati ya kufuatilia, ikiwa ni pamoja na kuanzisha mfumo "database" ili kugundua wanaofanya udanganyifu.<br><br>Aidha wizara ilimuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kufanya uchunguzi juu ya suala hili na ripoti yake tayari imewaslishwa kwa Mhe. Rais.<br><br>Vile vile wizara inakusudia kuomba msaada kutika shirika la kazi "ILO" katika kupata mfumo ambao utawasaidia kutatua changamoto hizo. | Kamati imeomba watendaji waliohusika kufanya udanganyifu wachukuliwe hatua. Aidha Kamati imeiomba Kamati ya kisekata, ilifuatilie zaidi suala hili, kwa kushrikiana na Wizara husika kwa kufanya uhakiki kwa kila wilaya. | |
| 3. | Wajumbe wengi walichangia kuhusu Bajeti ya Mabaraza ya vijana kuwa ni ndogo sana ambapo kwa mwaka wa fedha **2017/2018**, Mabaraza ya vijana yote ambayo takriban yapo 52 ngazi ya Shehia, 11 ngazi ya Wilaya na | Wizara ilieleza kuwa, fedha hizo hazikutengwa kwa ngazi ya wilaya, na shehia, isipokuwa zilitengwa kwa ngazi ya taifa, kwa ajili ya shughuli za uratibu kupitia Katibu mtendaji kwa ajili ya shughuli za uratibu ngazi ya | Kamati imeridhia bajeti hiyo ibakie kama ilivyo, kwa masharti kwamba Wizara ihakikishe fedha hizo zinatumika kwa mujibu wa malengo yaliyowekwa. | Hakuna fedha iliyoongezwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 1 ngazi ya Taifa yametengewa Tsh **100,000,000** tu ambazo kimsingi haziyawezeshi Mabaraza hayo kutekeleza shughuli zake ipasavyo | Taifa na kusukuma maendeleo ya mabaraza ya vijana.<br><br>Aidha, Wizara imeeleza kuwa, zipo program nyengine za Wizara, ambazo zinasaidia masuala ya vijana kwa ujumla.<br><br>Kwa kuwa utaratibu wa Baraza la vijana bado ni mpya, Wizara imeomba waachiwe fedha hizi kama zilivyopangwa ili kuangalia ufanisi wake. | Aidha Kamati imeitaka Wizara katika bajeti ya mwaka ujao, itoe maelezo juu ya shughuli gani imefanyika kwa bajeti hiyo na iwapo imefikia lengo. | |
| | | | | |
| | **WIZARA YA ELIMU:FUNGU KO1** | | | |
| 1. | Kwakuwa suala la elimu ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali na kwakuwa kuna mahitaji mengi ya wanafunzi wanaohitaji mikopo ya elimu ya juu, ambapo wengi wao wanakosa mikopo hiyo, Wajumbe wamependekeza fungu la Mikopo ya Elimu ya juu liongezwe ili kuweza kuongeza idadi ya wanafunzi | Wizara imeeleza kuwa, kwa mwaka huu wa fedha, kasma hiyo imeongezeka, kulinganisha na bajeti ya mwaka 2016/2017. Aidha Wizara imeeleza kuwa, fedha hizo kwa mwaka huu wa fedha hazitawanufaisha wafanya kazi wa Serikali.<br><br>Sambamba na ongezeko hilo, kwa mwaka huu wa | Kamati imeishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango, kuhakikisha kuwa, fedha zinaingizwa kwa wakati ili wanafunzi wasipate usumbufu wakati wa masomo. | Hakuna fedha iliyoongezwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | wanaonufaika na huduma hiyo. Kwa mwaka wa fedha **2017/2018** huduma hiyo imepangiwa Tsh **10,203,700,000.** | fedha, mbali na gharama za masomo (ada), Wizara pia itawapatia wanafunzi fedha za kujikimu (posho) ambapo jumla ya wanafunzi 1600 wapya watanufaika na mkopo huo. | | |
| 2. | Wajumbe wengi wamezunguzmzia suala la kumalizia majengo ya Skuli ambayo wananchi wamejitolea kuyajenga | Wizara imekiri kuwepo kwa tatizo hilo, na kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tayari fedha zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha jumla ya madarasa 285.<br><br>Aidha kuna wafadhili mbali mbali wameahidi kusaidia suala hili ikiwa ni pamoja na Jumuiya ya *"Milele Foundation"* | Kamati imeridhika na majibu ya Wizara, lakini pia imeitaka Kamati ya kisekta ifuatilie utekeleaji wa suala hilo. | |
| | | | | |
| 3. | Wajumbe wamependekeza kuwa fedha zinazochangishwa kwa ajili ya ununuzi wa madawati zisiekwe benki, bali zianze kutumika kwa matumizi yaliyokusudiwa, ili kuepuka kuongezeka kwa gharama za utengenezaji. | Wizara imeeleza kuwa, kutokana na kuwepo kwa changamoto ya uchache wa madrasa, imeona ni vyema kwanza kukamilisha ujenzi wa madarasa hayo kabla ya ununuzi wa madawati, ambayo yakinunuliwa kabla ya kuwepo kwa madarasa | Kamati imeridhika na maelezo ya Serikali | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ya kutosha itapelekea changamoto nyengine kwa kukosa sehemu ya kuyaweka. | | |
| | | | | |
| | WIZARA YA KILIMO: FUNGU L01 | | | |
| 1. | Kuhusu Soko la Kinyasini amabalo lilitengewa bilioni **2,500,000,000** na lilitarajiwa liwe tayari kwa miezi 6. Aidha, soko hilo lilitakiwa liwe la ghorofa mbili , liwe la kisasa, na liwe na *lift* tofauti na ilivyo kwa sasa ambapo linaonekana kuwa ni la kawaida | Wizara imeeleza kuwa, kwa mujibu wa makubaliano ya wafadhili na Halmashauri husika, jengo hilo liliafikiwa kuwa liwe la kawaida (la chini) lakini msingi (foundation) wake uwe na uwezo wa kujengewa ghorofa tatu.<br><br>Aidha kwasababu halina ghorofa kutokana na makubaliano hayo, fedha za "lift" zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa uzio pamoja na kuongezea idadi ya vyoo.<br><br>Aidha jengo limechelewa kumaliza kutokana na kuwepo kwa chagamoto ya upatikanaji wa vifaa. | Kwa kuwa fedha zilizotumika kwa mradi huo ni nyingi, Kamati imeishauri Kamati ya kisekta kufuatilia kwa karibu ujenzi huo. | |
| 2. | Wajumbe wengi | Wizara imeeleza kuwa, ipo | Kamati imeshauri | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | wamechangia kuhusu suala la mchanga kutokana na uamuzi wa Serikali kuyachukua Mashamba ya Mchanga yaliyokuwa yanamilikiwa na watu binafsi bila ya kulipiwa fidia. Aidha, Wajumbe wamesikitishwa na bei kubwa wanayouziwa wananchi kinyume na bei elekezi iliyotolewa na Serikali. | tayari kulipa fidia, iwapo mdai atakuja na nyaraka halali zitakazo halalisha madai yake.<br><br>Aidha, kimsingi Serikali haijaongeza bei ya mchanga, lakini ongezeko hilo linasababishwa na wafanyabishara kutokana na kutokukubaliana na utaratibu uliowekwa na Serikali. | Serikali iondoe zamu za kwenda kuchukua mchanga mashimoni ikiwa ni moja ya sababu inayopelekea wafanya biashara kupandisha bei ya mchanga.<br><br>Aidha, Serikali imeshauriwa kutoa elimu kwa wananchi, kuhusiana na rasilimali hiyo na umuhimu wa kudhibiti matumizi yake. | |
| | | | | |
| | **WIZARA YA BIASHARA VIWANDA NA MASOKO: FUNGU R01** | | | |
| 1. | Imependekezwa kuwa, kianzio cha Mapato cha Mali Maiti ambacho kwa sasa kipo chini ya Wizara ya Biashara Kihamishiwe Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ambayo ipo chini ya Wizara ya Katiba, Sheria , utumishi wa Umma na Utawala Bora | Wizara imeeleza kuwa, tayari imeanza kulichukulia hatua suala hilo, kwa kuwaandikia Wizara ya Katiba Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuhusu kukirejesha kitengo hicho. | Kwakuwa chanzo hicho hakihusiani moja kwa kwa moja na Dini ya Kiisalm, Kamati imeshauri kuwa, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Wizara ya Katiba, na Wizara ya Biashara, wakae pamoja na kushauriana juu ya kitengo muafaka cha kukiweka chanzo hicho | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | cha mapato. | |
| | | | | |
| | **WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI: FUNGU P01** | | | |
| 1. | **Wajue wengi,** hawakuridhishwa na **Maendeleo ya Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Termina II wa A.A. Karume International Airport** ambao umechukua zaidi ya miaka mitano. Aidha, Wajumbe wengi wakati wakichangia bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, wameonesha kutoridhishwa<br><br>na mradi huo, ambao umekuwa wa muda mrefu na umegharimu Serikali fedha nyingi. Pia Wajumbe wameitaka Serikali kuwachukulia hatua waliohusikana na uzembe katika kadhia hiyo. | Kimsingi, Serikali imeeleza kuwa kwa sasa mkwamo wa mradi huo umeshapata uatatuzi, ambapo wafadhili (Exim Bank) wamekubali kuingiza fedha ili kuendeleza mradi huo, ambapo mradi unatarajiwa kuendelea ndani ya mwaka huu wa fedha. | Kamati imeshauri katika ujenzi wa Terminal hiyo kuzingatiwe kujengwa kwa mfumo wa kutiririsha maji, ili kuepuka kutuama kwa maji katika eneo hilo.<br><br>Aidha, kwakuwa mradi huo ni wa siku nyingi na umeigharimu Serikali fedha nyingi Kamati ya Bajeti imekukusudia kuufuatlia mradi huo. | |
| 2. | Fungu la Idara ya Utunzaji wa Barabara UUB liongezwe ili Idara hii iweze kufanya kazi kwa ufanisi, kwa kuzitengeneza barabara zilizoharibiwa na mvua za masika. Aidha kutokana na ubovu wa barabara nyingi, Wajumbe wengi wameonesha hofu juu ya Wakandarasi wanaopewa tenda za ujenzi wa barabara | Wizara imeeleza ina mpango wa kuanzisha viwango "standard" vyake maalum vya ujenzi wa barabara ambavyo vitafuatwa na wakandarasi wote wa barabara au wakati wa ujenzi wa barabara. | Kamati imimemshauri Mwenyekiti wa Kamati ya Kisekta afuatilie kwa karibu ufanisi wa Idara hiyo. | Hakuna fedha iliyoongez wa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | ambazo mara nyingi huwa zinakosa viwango. Hivyo Wajumbe wameitaka Serikali kuangalia uwezekano wa kuitumia Idara ya UUB ili iweze kutengeneza barara badala ya kutegemea wakandarasi wa nje ambao hawana viwango | Aidha, serikali ina mpango wa kuwa na mamlaka ya barabara ambayo itafanya kazi sawa na zinazofanywa na "TanRod" kwa Tanzania bara.<br><br>Vie vile wizara ilieleza kuwa fedha hiyo ni zaidi ya bajetiiliyopangwa kwa mwaka 2016/2017, hivyo kwa ujumla fedha hizo zinatosheleza mhahitaji ya Idara hiyo. | | |
| 3. | Kamati ya Ardhi na Mawasiliano imependekeza bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji iongezwe ili waweze kukabili changamoto nyingi zinazowakabili zikiwemo zile za ubovu na uchakavu wa majengo ya nyumba za taasisi zake, uhaba wa vitendea kazi, uhaba wa usafiri kwa ajili ya Idara mbali mbali. | Wizara imeeleza kwamba kimsingi hawana chanagamoto ya vitendea kazi, badala yake walikuwa na tatizo la "maintenance" hata hivyo kwa mujbu wa bajei walyopangiwa mwaka huu wanatarajia chngamoto hiyo itaweaa kutatuka. | Kamati imeridhika na majibu | Hakuna fedha iliyoongez wa |
| | **WIZARA YA AFYA** | | | |
| 1. | Katika fungu ka Huduma za Ufatiliaji wa Maradhi Yasiyoambukiza liliopo Wizara ya Afya kwenye | Wizara imeeleza kwamba usasahihi wa fedha hizo ni kama amabavyo zimeoneshwa kwnye kitabu | Kamati imeridhika na maelezo ya Wizara | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | kitabu kikubwa cha bajeti imetengwa milioni 30,000,000 makisio yake lakini kwenye fedha ya maendeleo hakuna kitu iko zero na kwenye kitabu kidogo. Kinaonesha zimetengwa milioni 96,000,000 lakini na maendeleo ni 2,865,967,000 | kikubwa "estimate book" | | |
| | | | | |
| | **WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI MAJI NA NISHATI** | | | |
| | | | | |
| 2. | Ili kuiokoa ZECO na kubeba mzigo mkubwa wa madeni imependekezwa Wizara ya Fedha kulipa moja kwa moja ZECO huduma ya umeme kwa zile taasisi ambazo hazijaungiwa mita za tukuza ili kulipa nguvu Shirika kuweza kutoa huduma bora kwa wakati na pia kuweza kulipa madeni ya TANESCO | Katika kukabiliana na chanagamoto hiyo ZECO imeanzisha utaratibu maalum wa kuzifungia mita za Tukuza taasisi za Serikali Aidha, Wizara imeeleza kua, Serikali ina mkakati maalum wa kuhakikisha inamalza madeni ya taasisi zake. Yanayodaiwa na ZECO, pamoja na deni la zamani, inalodaiwa na Tanesco ambapo kwa sasa serikali kupitia ZECO inalipa jumla ya Tsh 4.5 bilioni kila mwezi ili kuhakikisha hailimbikizi deni jipya kwa TANESCO.<br><br>Aidha, kuhusiana na madeni ya Umeme wanayodaiwa Viongozi Wakuu, Wizara ilileleza kuwa malimbikizo ya | Kamati imeridhiswa na maelezo yaliyotolewa na Wizara kuhusu mikakati ya Serikali kumaliza deni lake la moda mrefu kwa TANESCO, na madeni ya taasisi zake kwa ZECO.<br><br>Kuhusiana na madeni ya viongozi wakuu, Kmati imeagiza kupatiwa vilelezo kutoka Wizara husika vinayothibitisha kuwa madeni yote wanayodaiwa Viongozi | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Madeni yote tayari yameshalipwa na kwa sasa hakuna Kiongzi Mkuu anaedaiwa. | Wakuu yamelipwa. | |

**Hitimisho**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia napenda kukushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha majumuisho ya mjadala wa makadirio ya bajeti. Aidha napenda pia kuwashukuru wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa makini wakati nikiwasilisha majumuisho ya Kamati ya bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndg. Raya Issa Msellem pamoja na wasiadizi wake kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake vizuri.

Ahsante, Naomba kuwasilisha.

Mohammed Said Mohammed (Dimwa)

Mweyekiti,

Kamati ya Bajeti,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**